

# Udongo Bora, Kwa Mavuno Endelevu

## Chukua Hatua Sasa

Kuboresha afya ya udongo ni suluhisho la msingi la mabadiliko ya tabianchi.









## KILA HATUA INA MAANA

**Anza kwenye udongo!**

- Asilimia 40% ya udongo duniani tayari umeharibika
- Udongo wenye afya huhifadhi kaboni zaidi na huongeza mavuno
- Udongo mzuri husaidia kuhifadhi maji na kupunguza athari za ukame

Kuwa sehemu ya kampeni ya AFYA YA UDONGO ya Shirika la Maendeleo ya Kilimo Njombe (NADO)

Kama utahitaji kufahamu au kupata msaada zaidi wa mafunzo ya mbinu za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, wasiliana na NADO

Piga Simu: 0756 000 387/0763 204 364/0758 156 477 Baruapepe: info@nado.or.tz

YouTube: NJOMBE AGRICULTURAL DEVELOPMENT ORGANIZATION

Instagram: nado_tanzania

Facebook: NJOMBE AGRICULTURAL DEVELOPMENT ORGANIZATION

www.nado.or.tz

NJOMBE AGRICULTURAL DEVELOPMENT ORGANIZATION — NADO — UBIA, UMOJA

A5 Flyer Soil.indd 1 8/21/2025 9:20:49 PM


# WAKULIMA wanawezaje kupambana na mabadiliko ya TABIA NCHI?



**Wakulima wanaweza:**

- Kutumia mboji na samadi asilia kuboresha rutuba.
- Kufanya mzunguko wa mazao ili kusawazisha virutubisho vya udongo.
- Kupanda mazao funika ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.
- Kulima kilimo mseto (agroforestry) ili kuongeza kivuli na unyevu shambani.
- Kuepuka kuchoma mashamba ili kulinda viumbe wa udongo.
- Kutumia mkaa mazao (biochar) ili kupunguza uchachu/tindikali kwenye udongo.

## AFYA YA UDONGO










> *"Tangu nianze kutumia samadi, mavuno yangu yameongezeka mara mbili—na udongo wangu hubaki na unyevu hata wakati wa kiangazi!"*
>
> *Elisha Mgaya - Mkulima, Kijiji cha Nyumbanitu, Njombe*

**NADO (kupitia Mradi wa FORI) inashirikiana na wakulima wa mkoa wa Njombe kukuza mbinu endelevu za utunzaji wa udongo na kupambana na mabadiliko ya tabianchi kupitia elimu, mashamba ya mafunzo, na ushirikiano na wataalamu wa kilimo na mifugo.**

Mradi umefadhiliwa na:

Mradi umetekelezwa na:

Kipeperushi hiki kimetayarishwa kwa ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya (EU) na OACPS. Maoni yaliyomo kwenye kipeperushi hiki hayaakisi maoni rasmi ya Umoja wa Ulaya (EU) au OACPS.